

JUZUU 2

PAMOJA NA WATOTO



PLAY KIT
YA KUJIFUNZA

SETI YA KUCHEZA NA KUJIFUNZA NYUMBANI NA SHULENI

WACHA TUANZE

Jedwali La Yaliyomo

Michezo Kumi ya Kucheza

1. Kuigiza
2. Mchezo wa kukimbia na Kitu
3. Wanyama Kutumia Maumbo
4. Nakudhubutu
5. Kutunga Hadithi Pamoja
6. Lenga Chupa ya Maji
7. Vikaragosi vya Vijiti
8. Maonyesho ya Vikaragosi
9. Tengeza Fumbo
10. Tengeza Gari la Kuchezea

1

Habari!

Karibu kwenye PLAYKIT yako mpya.
Tumefurahi sana kukutana nawe. Tumekutengenezea
michezo 10 ya kufurahisha ili ucheze na watoto wako.
Je, umefurahia?
Haya ni baadhi vidokezo.



2


Upande wetu wa kushoto ni jedwali yaliyomo
na orodha ya michezo unayoweza kucheza.

Pia utaweza kuwazawadia watoto wako beji 2
nzuri: moja ukimaliza na michezo 5 ya kwanza
na ya mwisho baada ya kukamilisha yote 10.
Vizuri sana! Sivyo?



3

Umelewa Kila kitu?
Tuanze mchezo!



01 KUIGIZA


VIFAA:

Kadi za Maneno Zilizokatwa
Kutoka kwa Kiolezo,
Kadi Tupu za Kuongeza Maneno


SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Lugha na Kusoma
(Kiingereza au Kiswahili)

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Dakika 30



1

Mtoto mmoja achukue
kadi na asionyeshe mtu
mwingine yeyote



2

Mtoto huyu ajaribu kuwafanya wengine
kukisia neno lililo kwenye kadi kwa kuigiza
nenosililo kwenye kadi na kutumia miondoko
ya mili yao. Mtoto lazima ajaribu kufanya
hivyo bila kuongea.



3

Wacha kila mmoja
aweze kuchagua kadi
kwa zamu.




**Matokeo
ya Mwisho**



TUK TUK




NGOMA



NDEGE



UVUVI



JAHAZI



BODA BODA




**MCHEZO : Kuigiza
Tengeneza nakala na ukate kwenye mstari wa vitone na utumie kadi kwa shughuli ya 'Igize'**

NDOVU



PUNDA



**MSANII MAARUFU WA
MUZIKI AFRIKA
MASHARIKI**



Diamond Platnumz

SIMBA



KANDANDA



**KUCHEZA
DANSI**



MCHEZO : Ku igiza
Tengeneza nakala na ukate kwenye mstari wa vitone na utumie kadi kwa shughuli ya 'Igize'

02 MCHEZO WA KUKIMBIA NA KITU

VIFAA:

Mikebe au Ndoo Nne Ndogo ,
Vikombe Viwili, Maji au Mchanga

SEHEMU YA KUJIFUNZA:


Sanaa ya Ubunifu na Harakati

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



1

Tengeza timu mbili na zisimame
kwa mstari. Weka ndoo iliyojaa
Maji mbele ya kila timu



2

Panga ndoo tupu umbali wa futi
20 mbele ya kila timu



3

Mpe mtoto aliye mbele
ya mstari kikombe ashikilie



4

Mtoto aliye mbele achote maji kisha
akimbie akamimine kwenye ndoo tupu na
arudi kumpokeza mwenzake kikombe hicho



5

Timu ya kwanza itakayo
jaza ndoo itakua imeshinda

**Matokeo
ya Mwisho**



03 WANYAMA KUTUMIA MAUMBO

VIFAA:

Karatasi, Makasi, Penseli, Gamu
ama Gundi


SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Hesabu

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:




Saa 1




1

Chagua mnyama
unayetaka kutengeza




2

Chora maumbo tofauti kwa mfano
Mstatili, Pembe tatu, Duara, N.k



3

Kata maumbo
uliyochora



4

Unganisha maumbo pamoja kutengeza
mnyama uliyemchagua



Matokeo ya Mwisho

VIFAA:

Karatasi, Makasi, Kalamu ya rangi kijani [Green], Gundu [gamu], Rangi ya hudhurungi [Brown]{ukipenda}, Brashi ya kupaka rangi


SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sanaa ya Ubunifu na Harakati

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Saa 1



1

Shina la mti: Kunja karatasi mviringo na uunganishe kwa gundi.



2

Paka mviringo huo rangi ya hudhurungi kisha wacha ikauke kwa muda (Ukipenda)



3

Sehemu ya juu ya mti:
Kata karatasi kwa wembamba kutengeza majani




4

Vipake vipande hivyo rangi ya kijani



5

Viunganishe vipande hivyo vya majani kwenye shina la mti.



6

Andika mchezo mmoja kwa kila jani. Iwapo mtoto atachagua jani ita afanye agizo.
Hii ni baadhi ya mifano ya michezo na unaweza kutengeza yako mwenyewe:

- Nguruma kama simba
- Imba wimbo wa alfabeti kutoka mwisho hadi mwanzo[z-a].
- Jifanye wewe ni twiga au ndovu n.k.
- Cheza wimbo
- Funga macho na ubahatishe anayetingisha mkono wako[mwalimu atachagua mtoto mwengine]
- Ruka kwa mguu mmoja

**Matokeo
ya Mwisho**



05 KUTUNGA HADITHI PAMOJA


VIFAA:

Herufi za Alfabeti


SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Lugha na Kusoma
(Kiingereza au Kiswahili)

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:




Dakika 30



1

Kata herufi



2

Mpe kila mtoto herufi

Herufi A: Niliamka
asubuhi moja na
kupata

3



Uliza mtoto mmoja kuanza kusimulia
hadithi kulingana na herufi yao.
Kisha kila mtoto aendelee hadithi
hiyo kwa kuiongeza kwa kutumia
herufi walioshikilia

KWA MFANO

Herufi A: Niliamka asubuhi moja na
kupata

Herufi S: Simba kitandani

Herufi T: Tumbo lake lilikuwa


linatengeneza kelele hivyo niiuliza

Herufi K: Je, ungependa kuku


Matokeo ya Mwisho

Herufi M: nilikuwa
na urefu Mara
Mbili ya jana






Ee




Jj




Dd



Ii




Cc




Hh




Bb




Gg




Aa




Ff




Oo




Tt




Nn




Ss



Mm




Rr




Ll




Qq




Kk



Pp



Yy



Xx



Ww



Vv



Uu



Zz

06 LENGA CHUPA YA MAJI

VIFAA:

Mpira, Chupa 10 za Plastiki, Maji , Kokoto au Mchanga


SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sanaa ya Ubunifu na Harakati

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



Saa 1




1

Weka maji, mchanga
ama kokoto nusu kwa
kila chupa




2

Panga chupa za maji
au wanyama wa maumbo
halisia kwa msitari



3

Shika mpira, simama
hatua kumi na ulekee
chupa



4

Bingirisha mpira uangushe chupa
nyingi uwenzavyo

Matokeo ya Mwisho



07 VIKARAGOSI VYA VIJITI

VIFAA:

Karatasi, Kalamu za Rangi,
Makasi, Vijiti, Tepu ama Gamu

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sanaa ya Ubunifu na Harakati

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:




Saa 1




1

Chora kikaragosi kwenye
karatasi na utengeze uso.
Inaweza kuwa mtu au mnyama




2

Paka rangi



3

Kata kikaragosi



4

Unganisha kikaragosi chako
kwenye kijiti

**Matokeo
ya Mwisho**



08 MAONYESHO YA VIKARAGOSI

VIFAA:

Vikaragosi Vya Vijiti

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Lugha na Kusoma
(Kiingereza au Kiswahili)

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:




Saa 1



1

Chagua hadithi inayojulikana
(Kwa mfano, Sungura na Kobe)



2

Tengeza vikaragosi kuwakilisha wahusika tofauti katika hadithi hio



3

Wahusika wanafanya nini kwenye hadithi?
Ni yapi majina ya wahusika?



4

Shirikianeni kucheza mchezo na kujaribu sauti tofauti tofauti



Matokeo ya Mwisho

09 TENGEZA FUMBO

VIFAA:

Karatasi au Boksi, Kalamu za Rangi, Makasi

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sanaa ya Ubunifu na Harakati

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:




1

Chora sehemu sehemu ya hadithi uliyopenda zaidi kwenye karatasi. Mchoro ujaze karatasi



2

Paka rangi picha ile



3

Kata vipande kadhaa karatasi ile; vinaweza kuwa maumbo tofauti kama mstatili au Pembe tatu



4


Vichanganye vipande vile kwa mfuko



4

Badilishaneni vipande vile kwa ajili ya kupanga kurudisha muonekano wa picha ya awali.

**Matokeo
ya Mwisho**



10 TENGEZA GARI LA KUCHEZEA

VIFAA:

Chupa ya Plastiki, Vifuniko 4 vya
Chupa, Vijiti 2 vya Mbao, Kisu au
Makasi, Kamba

SEHEMU YA KUJIFUNZA:

Sayansi na Teknolojia

MAELEKEZO YA JINSI YA KUCHEZA:



1




Safisha chupa ya plastiki

2




Kata mashimo mawili katika kila
upande wa chupa

3



Weka vijiti kuititia kwa mashimo. Toboa
shimo ndogo katika kila kifuniko cha
chupa na uziambatishe kwenyevijiti

4




Kata kidogo sehemu ya juu ya chupa
baada ya kuweka magurudumu
(ili kuwa na nafasi ya viti au kubeba vitu)

5

Funga kamba katika sehemu ya juu ya chupa.
Livute gari kwa kutumia kamba

Matokeo ya Mwisho



**SHUGHULI
ZA MICHEZO
BEJI ZA MCHEZO**

>>

HONGERA!

Kwa mtoto wako anayepata beji yake ya kwanza

BEJI: Ninapata kupika chakula cha jioni na mama au baba yangu

Kata na uvae mojawapo ya beji hizi za michezo kwa kujivunia



HONGERA!

Kwa kupata beji yako ya pili

BEJI: Ninapata kuunda mchezo mpya wa kucheza na wazazi

Kata na uvae mojawapo ya beji hizi za michezo kwa kujivunia





JUZUU 1
WATOTO



JUZUU 2
PAMOJA NA WATOTO

PLAY KIT

YA KUJIFUNZA

SETI YA KUCHEZA NA KUJIFUNZA NYUMBANI NA SHULENI